**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA KWANZA

**26 JANUARI, 2016**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA PILI

## KIKAO CHA KWANZA – TAREHE 26 JANUARI, 2016

Wimbo wa Taifa Kuimbwa, Dua Kusomwa na Kikao Kuanza Saa Tatu Asubuhi.

## I. KIAPO CHA UAMINIFU:

Orodha ya Wabunge watakaoapishwa:-

1. Mhe. Abdallah Saleh Possi, Dkt.
2. Mhe. Deogratias Francis Ngalawa
3. Mhe. Godbless Jonathan Lema
4. Mhe. Goodluck Asaph Mlinga
5. Mhe. Makame Mnyaa Mbarawa Prof.
6. Mhe. Omari Abdallah Kigoda
7. Mhe. Philip Isdor Mpango, Dkt.
8. Mhe. Rashid Mohammed Chuachua
9. Mhe. Shabani Omari Shekilindi

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI MKUU:**

Taarifa ya Matoleo ya Gazeti la Serikali pamoja na Nyongeza zake zilizochapishwa tangu tarehe 4 Novemba, 2015 kama ifuatavyo:-

(i) Toleo Na. 49 la tarehe 04 Novemba, 2015
(ii) Toleo Na. 06 la tarehe 06 Novemba, 2015
(iii) Toleo Na. 50 la tarehe 11 Novemba, 2015
(iv) Toleo Na. 13 la tarehe 13 Novemba, 2015
(v) Toleo Na. 51 la tarehe 18 Novemba, 2015
(vi) Toleo Na. 47 la tarehe 20 Novemba, 2015
(vii) Toleo Na. 52 la tarehe 25 Novemba, 2015
(viii) Toleo Na. 08 la tarehe 27 Novemba, 2015
(ix) Toleo Na. 01 la tarehe 01 Januari, 2016
(x) Toleo Na. 02 la tarehe 08 Januari, 2016

## III. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**1. MHESHIMIWA GEORGE MALIMA LUBELEJE (MPWAPWA) :**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa wanakabiliwa na tatizo kubwa sana la njaa; na katika msimu wa mwaka 2014/2015 mvua hazikunyesha kabisa na kusababisha wananchi wengi kukosa chakula kutokana na ukame; na Serikali imekwisha tamka

kwamba hakuna mwananchi atakayekufa kwa njaa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza kugawa chakula cha njaa Wilaya ya Mpwapwa.

**2. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Tatizo la ajira Nchini kwa wahitimu wa Vyuo vya kati na vya juu ni kubwa sana:-

(a) Je, ni wahitimu wangapi hawana kazi hadi sasa kutoka Vyuo vya Elimu ya Juu Nchini;

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ajira kwa wahitimu hao au kuwawezesha kujiajiri hasa vijana.

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI)**:

**3. MHESHIMIWA AZZA HILLAL HAMAD (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Mradi wa maji wa kisima kirefu katika mji mdogo wa Tinde umechukua muda mrefu sana kukamilika:-

Je, ni lini sasa mradi huo utakamilika.

4. **MHESHIMIWA RASHID ABDALLAH SHANGAZI (MLALO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaharakisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wakazi wa kata za Manolo, Shume, Sunga na Mbaru ili kuwaondolea usumbufu Wananchi wa maeneo hayo ikiwamo ushiriki hafifu kwenye shughuli za kiuchumi.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

5. **MHESHIMIWA MARYAM SALUM MSABAHA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-
Kumekuwa na ongezeko la watoto wanaoishi katika mazingira magumu katika miji mikubwa kama Dar es Salaam, Arusha, Mbeya, Dodoma, Mwanza n.k watoto hawa wengi wao hawaendi shule na kazi yao ni kuomba omba barabarani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha watoto hao wanarudishwa shuleni kusoma;

(b) Je, ni lini Serikali itawachukulia hatua wale wote wanaowatumia watoto hao kuomba omba.

**6. MHESHIMIWA MAFTAHA ABDALLAH NACHUMA (MTWARA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:- Serikali kwa miaka mingi imekuwa na mpango wa kujenga hospitali za Rufaa za Kanda; na tayari Kanda zote zina hospitali hizo isipokuwa Kanda ya Kusini tu:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanza kujenga hospitali hiyo Kanda ya Kusini ambapo tayari eneo la Mitengo Mikindani limetengwa kwa zaidi ya miaka saba na hakuna kinachoendelea;

(b) Je, Serikali haioni kuwa haiwatendei haki Wananchi wa maeneo ya Kanda ya Kusini kama Wananchi wa maeneo mengine.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**7. MHESHIMIWA ANNA RICHARD LUPEMBE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Ujenzi wa barabara ya Sumbawanga hadi Mpanda bado haujakamilika:-

Je, ni lini ujenzi wa barabara hiyo utakamilika.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

**8. MHESHIMIWA DKT. FAUSTINE ENGELBERT NDUGULILE (KIGAMBONI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi:- Hapa Tanzania kumekuwepo na migogoro mbalimbali ya ardhi kati ya wawekezaji na Wananchi, wakulima na wafugaji, Hifadhi na Wananchi na baina ya Wananchi wenyewe:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya kupanga matumizi bora na endelevu ya ardhi ili kuondokana na migogoro;

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuondokana na tatizo la Maendeleo ya miji kutokuendana na kasi ya ukuaji wa miji.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**9. MHESHIMIWA MARWA RYOBA CHACHA (SERENGETI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:- Kumekuwepo na uvamizi wa Tembo kutoka Hifadhi ya Serengeti na kusababisha vifo na uharibifu wa mashamba katika Wilaya ya Serengeti na maeneo jirani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kunusuru maisha na mali za wananchi waishio Serengeti;

(b) Je, Serikali ina mpango wa kutathmini upya fidia inayotolewa kwani haiendani na hali halisi ya uharibifu wa mali na upotevu wa maisha ya watu.

**WIZARA YA NISHATI NA MADINI:**

**10. MHESHIMIWA JOHN WEGESA HECHE (TARIME VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini:- Tathmini ya Mgodi wa Nyamongo (ACACIA) kwa wakazi wa Vijiji vya Nyakunguru, Kewanja, Nyangoto, Matongo kupisha upanuzi wa uzalishaji wa mgodi ilifanyika kuanzia mwaka 2012 ambapo wananchi walizuiwa kuendeleza maeneo yao :-

(a) Je, Wananchi hao watapewa lini fidia kutokana na maeneo yao kulingana na bei ya sasa ;

(b) Je, fidia hiyo itaendana na usumbufu na hasara waliyoipata hadi sasa.

## WIZARA YA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

**11. MHESHIMIWA MATTAR ALI SALUM (SHAURIMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa:- Kikosi cha Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) huandaa vijana kwa mafunzo mbali mbali kwa ajili ya kusubiri ajira katika vikosi vya ulinzi vya Muungano:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa utoaji ajira kwa upande wa Tanzania Zanzibar;

(b) Je, ni asilimia ngapi ya vijana wanaoajiriwa kutoka upande wa Zanzibar;

(c) Je, kwa nini utoaji wa ajira katika Wizara hii kwa upande wa Zanzibar usijielekeze kwenye kikosi cha kujenga uchumi (JKU) tu.

## WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:

**12. MHESHIMIWA FLATEI GREGORY MASSAY (MBULU VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani:- Kutokana na wizi wa mifugo uliokithiri katika Bonde la Yayeda Chini Serikali ilianzisha kituo cha Polisi na sasa kimeondolewa:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukirudisha kituo hicho ili wananchi wapate huduma za ulinzi wa mifugo na mali zao.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI, TEKNOLOJIA NA UFUNDI:**

**13. MHESHIMIWA RASHID ALI ABDALLAH (TUMBE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:- Kwa mujibu wa sheria, Wizara ya Fedha inatoa mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu nchini Tanzania:-

Je, ni utaratibu gani mzuri wa kuondoa usumbufu kwa wanafunzi kupata mikopo yao kwa wakati.

**14. MHESHIMIWA CECIL DAVID MWAMBE (NDANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi:-:

(a) Je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha wanafunzi hawarudishwi shule kwa sababu ya michango ya mlinzi, madawati na chaki;

(b) Je, Serikali ina mpango wa kuanzisha Chuo cha Ufundi (VETA) kwenye Jimbo la Ndanda.

**WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

**15. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji:- Wilaya ya Urambo imebahatika kuwa na Mto Ugalla unaopita Kusini kwake kuelekea Mto Malagarasi ukiwa na maji ya kutosha:-

Je, kwa nini Serikali isianzishe mradi wa kuvuta maji ya mto Ugalla kupeleka mji wa Urambo ambao unakua kwa haraka na Wananchi wake wamekuwa wakikabiliwa na uhaba mkubwa wa maji kwa muda mrefu.

## IV. KAULI ZA MAWAZIRI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA)**

## V. UCHAGUZI WA WENYEVITI WA BUNGE:

## VI. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI MKUU:**

Hoja ya kujadili Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoitoa wakati wa ufunguzi wa Bunge la Kumi na Moja, tarehe 20 Novemba, 2015.

**DODOMA** — **DKT. T. D. KASHILILAH**
**26 JANUARI, 2015** — **KATIBU WA BUNGE**